

MUONGOZO WA UOMBAJI WA UFADHILI WA ERASMUS MUNDUS SCHOLARSHIPS



Erasmus Mundus Joint Masters

Erasmus Mundus Joint Masters are delivered by multiple higher education institutions and run across various countries. They are distinguished by their academic excellence and by their high level of integration. Students at master's level from all over the world can apply.

Umetayarishwa na:

- ✚ Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika fani ya Uchumi wa Kilimo, Chuo kikuu cha Reading, Uingereza (MSc Agricultural Economics-University of Reading, UK) *ambaye pia ni;*
- ✚ Mnufaika wa Ufadhili wa Commonwealth (Commonwealth Masters Scholarships-2024) *ambaye pia ni;*
- ✚ Mfanyakazi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)

TANBIHI:

Maoni yaliyotolewa katika muongozo huu yanatokana na uzoefu wa mwandishi na wala sio maoni ya Kamati ya ufadhili wa Erasmus Mundus au Ofisi ya Umoja wa Ulaya.

Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa

©2024

YALIYOMO

UTANGULIZI WA MWANDISHI.	3
MAELEZO JUU YA UFADHILI WA ERASMUS MUNDUS SCHOLARSHIPS.	6
VIGEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA)	7
NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.	7
VIGEZO VYA UCHAGUZI (SELECTION PROCESS AND CRITERIA)	8
JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)?	8
NAMNA YA UOMBAJI HATUA KWA HATUA.	9
NAMNA YA KUANDIKA EMAIL (Professional email)	14
Sampuli ya Barua ya Utambulisho kutoka chuoni, (kama bado hujamaliza)	15
Sampuli ya Barua ya ngazi ya GPA-Class ranking kutoka chuoni, (kama itahitajika)	16
Sampuli ya Barua ya Motisha. Tafadhali usinakili maelezo haya katika barua yako, tumia kukuongoza tu. Iwapo utanakili ndio utakuwa umejinyonga mwenyewe.	17
Sampuli ya Uthibitisho wa makazi.	18
Sampuli ya barua ya mapendekezo (Recommendation letter).	19
Sampuli ya Wasifu binafsi (CV).	20
KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?	21
MIONGOZO MENGINE	22

UTANGULIZI WA MWANDISHI.

Ndugu watanzania wenzangu, tafadhali naomba mfahamu mambo kadhaa hasa katika kuomba ufadhili.

1. Kila ufadhili una vigezo vyake, hivyo unapaswa kujikita kwenye vigezo. Kuna baadhi ya ufadhili unaomba peke yake na chuo unaomba peke yake mfano Chevening, Commonwealth, Chinese Scholarship na kuna ufadhili unaomba na vyuo kwa pamoja katika ombi moja mfano Turkish Buslari scholarship, KNB Indonesian Scholarship na nyenginezo. Pia baadhi ya vigezo huwemo katika ufadhili Fulani na hukosekana kigezo hicho katika ufadhili fulani, mfano kigezo cha umri au uthibitisho wa ufasaha wa lugha ya kiingereza. Hivyo kabla ya kuanza maombi ya ufadhili au chuo husika, tafadhali pitia na soma maelekezo yote, hii itakusaidia kuwa na uhakika wa unachokifanya na kukuongezea nafasi ya kufanikiwa katika maombi yako.
2. Fadhili na vyuo vyingi duniani vinavyopokea wanafunzi wa kimataifa (International students) huweka maelekezo juu ya namna ya kuomba, au huweka majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara (Frequently Asked Questions-FAQs) au huweka mawasiliano yao iwapo utahitaji kuwasiliana nao. Tafadhali hakikisha unasoma maelekezo haya au unapitia FAQs, na ikibidi fanya mawasiliano nao iwapo utakwama au utapata changamoto yoyote.
3. Tafadhali fahamu kuwa fadhili nyingi huwa na ushindani wa hali ya juu, hivyo hakikisha unakidhi vigezo husika lakini pia unafata maelekezo husika kabla hujaanza kufanya maombi husika. Kusoma maelekezo husika kutakusaidia kutambua nini unafanya na hii itakupunguzia maswali au sintofahamu inayojitokeza wakati unafanya maombi yako.
4. Kufanya maombi ya Fadhili hata kama ni za kulipiwa kila kitu (Fully funded) mara nyingi huhusisha gharama kama vile muda na pesa. Mfano unaweza kutumia pesa katika kutoa nakala, kuthibitisha nakala zako kwa mwanasheria, kubadilisha nyaraka ngumu kuwa nyaraka laini (scanning), kuperuzi mtandao na mambo mengine. Unapaswa kutenga masaa kadhaa kila siku kupitia taarifa za scholarship na kuangalia kama una sifa.
5. **JIAMINI**, kama wengine walipata ufadhili, hata na wewe unao uwezo wa kupata. Muhimu ni **KUJITUMA** na kufuata maelekezo yote yanayotakiwa. Tafadhali pitia mfano wa uandishi wa email ambao nimeuainisha katika muongozo huu ili utumie kama njia ya mawasiliano iwapo utahitaji kufanya hivyo. Kumbuka kuwa mawasiliano kwa njia ya email ndio njia kuu ya mawasiliano kwa fadhili au vyuo vya nje ya nchi.

6. Usisahau kumtanguliza Mwenyezi Mungu kwenye kila kitu ufanyacho. Kwa hakika haswa utakutana na changamoto kadhaa, tafadhali usikate tamaaa. Hata wengine pia walikutana na changamoto wakati wanaomba. Siku zote amini kuwa, aliyewawezesha wengine kupata ndiye atakayekuwezesha wewe kupata.
7. Jihadhari na **utapeli**, kwenye uombaji wa ufadhili kuna utapeli pia hivyo hakikisha unahakiki ufadhili/chuo husika ili kuepuka kutapeliwa. Kumbuka kuwa si kila tangazo la ufadhili/udahili ni la kweli.
8. Epuka kunakili taarifa za mitandaoni na badala yake andika maandiko yako au ikibidi kuchukua taarifa za mtandaoni basi mtaje na muandishi ili kuepuka kosa la kunakili (plagiarism). Kuwa mkweli katika maelezo yako wakati unaandaa Wasifu binafsi (CV) au mpango wa masomo (Study plan) au barua ya motisha (motivational letter) au insha (essays). Mara nyingi uitwapo katika usaili, baadhi ya maswali huulizwa kulingana na taarifa ulizojaza katika nyaraka nilizotaja hapo awali, sasa kama umedanganya itakuwa vigumu kwako kujitetea.
9. Unashauriwa kuomba fadhili nyingi kadiri uwezavyo kulingana na vigezo unavyokidhi. Hata hivyo, ushauri wangu ni kuchagua fadhili zisizopungua 3 na zisizozidi 10 na kuhakikisha unazifatilia kwa umakini mkubwa sana. Kumbuka kuwa, kuomba fadhili nyingi bila kufata maelekezo husika au kukidhi vigezo husika hakukuongezei nafasi ya kupata badala yake nafasi ya kupata inaongezeka iwapo utafata maelekezo/vigezo husika hata kama utaomba ufadhili mmoja tu. (Hoja sio wingi wa kuomba fadhili nyingi, bali kinachosisitizwa ni kufata maelekezo husika kisha kuomba fadhili husika)
10. Tafadhali tambua kuwa uombaji wa fadhili au vyuo unahitaji umakini wako. Usiharakishe kutuma maombi kabla hujasoma maelekezo husika. Mfano, kuna baadhi yetu walifika mpaka chuo husika walichoomba wakidhani kuwa fadhili waliyopata ni ya kulipiwa kila kitu (fully funded) hali yakuwa ni ya kulipiwa baadhi (partially funded) na hivyo kupelekea kusoma kwa shida, kupata msongo wa mawazo na athari nyengine. Yasingewapata haya laiti wangelisoma maelekezo husika ya fadhili/chuo kabla ya kuomba.
11. Nafahamu UGUMU unaopatikana wakati wa kufatilia fadhili mbalimbali lakini JITAHIIDI ufanye maombi wewe mwenyewe na sio kufanyiwa na mtu au wakala. Hii itakurahisishia wakati wa usaili (interview) kwa kuwa utakuwa unajuwa ulichokiandika wakati unafanya maombi.

INDHARI: Lengo la muongozo huu ni kukupa mwanga wa namna ya kuomba ufadhili au chuo husika. Mwandishi hatoi huduma ya kufanyia watu maombi ya ufadhili wa aina yeyote ile, lakini yupo tayari kukusaidia pale utakapokwama kwa fadhili ambazo ana uzowefu nazo. Aidha maoni yaliyoandikwa humu hayatokani na taasisi au bodi ya ufadhili husika bali yanatokana na uzoefu wa mwandishi katika ufadhili husika.

USHAURI: Iwapo una maswali yahasuyo scholarship hii ya Erasmus mundus, tafadhali jiunge na group la WhatsApp la "Prospective EMA Tanzania" ambapo wanufaika wa scholarship hii wapo na watakusaidia kwa haraka zaidi. Wanufaika wana uzoefu zaidi juu ya scholarship hii kuliko muandishi wa muongozo huu. Kiunganishi cha kujiunga na group kipo katika ukurasa wa mwisho wa muongozo huu.

WananchiForum

MAELEZO JUU YA UFADHILI WA ERASMUS MUNDUS SCHOLARSHIPS.

UTANGULIZI.

Erasmus Mundus Scholarships ni miongoni mwa miradi ya Erasmus+ yenye lengo la kusaidia sekta ya Elimu, mafunzo, michezo na vijana inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU). Ufadhili huu unatoa fursa ya kusoma Shahada ya Uzamili (Masters) katika vyuo kadhaa vya Ulaya au nje ya Ulaya (vyuo vyenye mafungamano na vyuo vya Ulaya). Mara nyingi Master's kupitia ufadhili huu hutolewa kwa mashirikiano ya vyuo visivyopungua vitatu vya Ulaya (au nje ya Ulaya) na ndio maana Masters hizi huitwa Joint Master's (Erasmus Mundus Joint Masters-EMJM).

Ufadhili huu utakuwezesha kusoma Joint Master's itakayotolewa na chuo zaidi ya kimoja, ndani ya muda wa mwaka 1 au 2 (60, 90 or 120 [ECTS credits](#)) huku ukilipiwa gharama za usaviri, Visa na gharama za maisha kwa muda wote wa masomo.

Tafadhali tembelea kiunganishi hiki ili kusoma ushauri kwa waombaji <https://www.em-a.eu/>

Ufadhili huu ni miongoni mwa fadhili shindani duniani na ni miongoni mwa ufadhili wenye upekee kwa kuwa:

- ✚ Kila program (Master's) inatarehe zake za kuanza kupokea maombi na kufunga lakini mara nyingi huanza Octoba na kufungwa Januari (yamwaka unaofata) kila mwaka.
- ✚ Program (Master's) hiyo hiyo inapokea waombaji kupitia Erasmus na pia waombaji wanaojilipia wenyewe. Hivyo muombaji anatakiwa awe makini wakati anafanya maombi.
- ✚ Vigezo vya udahili hutofautiana kwa baadhi ya program (Master's) hivyo waombaji wanashauriwa kuzingatia vigezo husika katika program husika.
- ✚ Kila program (Master's) ina website yake ambayo itakupa maelekezo yote kuhusu namna ya kuomba ufadhili huu ikiwemo maelezo ya program husika, modules zake, vyuo husika vitakavyoshirikiana kutoa hiyo program, mahitajio na hatua za kufanya maombi husika.
- ✚ Ili kujua program (Master's) husika utapaswa kutembelea program catalogue kupitia link hii https://www.eacea.ec.europa.eu/scholarships/erasmus-mundus-catalogue_en ambapo hapo utatafuta program inayokufaa au inayoendana na wewe kisha aidha bonyeza jina la program husika au bonyeza website ya joint Master's. Website zote zitakuelekeza hatua unazotakiwa kufanya.

Baadhi ya faida za ufadhili huu ni pamoja na:

- ✚ Kusoma shahada ya uzamili ndani ya mwaka 1 au 2 katika zaidi ya vyuo vikuu 2 vya Ulaya
- ✚ Kulipiwa ada ya masomo
- ✚ Kulipiwa pesa za utafiti
- ✚ Kulipiwa gharama za usafiri.
- ✚ Kulipiwa gharama za Visa na bima ya afya

- ✚ Kulipiwa posho la kujikimu la kila mwezi uwapo Ulaya.
- ✚ Kushiriki matukio mbalimbali yatakayosimamiwa na Erasmus+
- ✚ Kuungana na wanufaika wengine wa Erasmus Mundus zaidi ya 50,000
- ✚ Kujifunza tamaduni mpya ya watu wa Ulaya au watu wengine wanufaika wa Erasmus Mundus

Mchakato wa ufadhili huu ni kama ifuatavyo:

Mchakato wa ufadhili huu upo tofauti kidogo na fadhili nyengine hivyo kila program ina mchakato wake. Hata hivyo jedwali lifuatalo linaonesha kwa ujumla namna mchakato unavofanyika:

Kufunguliwa kwa dirisha la maombi na kuanza kupokelewa kwa maombi ya ufadhili	Kuanzia Octoba, 2024
Kufungwa kwa dirisha la maombi na mwisho wa kupokelewa kwa maombi ya ufadhili.	Januari 2025.
Maombi huchakatwa ikiwemo kufanywa kwa usaili (interviews)	Kuanzia Novemba mpaka Machi 2025
Majibu ya ufadhili	Kuanzia Machi mpaka Juni 2025
Masomo huanza	Septemba 2025

VICEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA)

- ✚ Kuwa raia wa mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania.
- ✚ Kuwa na shahada ya awali au kuwa mwaka wa mwisho katika shahada ya awali ambapo utakuwa umemaliza ifikapo Septemba 2025.
- ✚ Kuwa tayari kuanza masomo ya Shahada ya Pili mwezi Sept 2025.
- ✚ Kutokuwa na uwezo wa kusoma shahada ya uzamili katika vyuo vya Ulaya.
- ✚ Kutuma nyaraka zote hitajika katika muundo uliopendekezwa.
- ✚ Baadhi ya vigezo hutegemea na program husika unayoomba hivyo fatilia vigezo vya program yako.

NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.

- ✚ Nyaraka za kitaaluma (Academic certificates and transcripts)
- ✚ Barua kutoka kwa wadhamini wawili wa kitaaluma (Two academic referees)
- ✚ Hati/pasi ya kusafiria
- ✚ Cheti cha lugha kama IELTS au TOEFL, au barua inayothibitisha kuwa ulisoma shahada ya awali kwa kiingereza (English proficiency letter)
- ✚ Barua ya motisha (Motivational letter)
- ✚ Uthibitisho wa makazi (Proof of residence) hii utaipata kutoka kwa Mwenyekiti au Sheha.
- ✚ Wasifu binafsi (CV)

VIGEZO VYA UCHAGUZI (SELECTION PROCESS AND CRITERIA)

Tafadhali zingatia kuwa mchakato huu kwa kuwa ndio utakaokusaidia kufanikiwa kupata ufadhili huu. Uchaguzi wa waombaji wa ufadhili huu hufanywa baada ya maombi ya waombaji hupewa alama (score graded) kulingana na vitu vifuatavyo:

- ✚ Uhodari wa kitaaluma (Academic merit)
- ✚ Ubora wa barua ya motisha (Motivational letters)
- ✚ Uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika nchi yako (Potential impact on the development (Sustainable Development Goals) of the candidate's home country- make sure you include this in your motivational letter and elaborate more during the interview)
- ✚ Barua 2 za mapendekezo (2 Recommendation letters)

JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTIHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)?

Jambo jema ni kuwa Ufadhili huu wa Erasmus Mundus hauna kigezo cha ulazima wa kuwa na cheti cha kuthibitisha ufasaha wa lugha ya kiingereza yaani IELTS au TOEFL kwa program nyingi. Hata hivyo, uandishi wako wakati unaandaa motivational letter au wakati wa interview utatumika kukupima uwezo wako katika kuandika na kufikisha ujumbe kwa kiingereza.

Aidha hata kwa vyuo ambavyo vitahitaji vyeti hivi vya ufasaha pia omba na tumia English proficiency letter kutoka chuo ulichosoma shahada ya awali.

Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu, masomo pamoja na mazingira yako yatakuwa ni kwa lugha ya kiingereza kwa asilimia zaidi ya 98 (kuna baadhi ya nchi utajifunza lugha ya nchi husika). Ni juu yako kuhakikisha unajua lugha hii kwa ufasaha ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima kama vile kufeli na msongo wa mawazo.

NAMNA YA UOMBAJI HATUA KWA HATUA

Fungua kiunganishi hiki ili kuanza maombi ya ufadhili huu

https://www.eacea.ec.europa.eu/scholarships/erasmus-mundus-catalogue_en

Utafunguka ukurasa wa course catalogue kama hivi:


The screenshot shows the Erasmus Mundus Catalogue homepage. On the left, there is a 'Filter by' section with dropdown menus for Keywords, Country, Duration and credits, Universities, Field of study, and Year of project selection. The main content area displays 'Erasmus Mundus Catalogue (189)' with an RSS feed icon. Below this, it says 'Showing results 1 to 20'. The first three results are: 'EMerald Master in Georesources Engineering' with URL 'https://www.em-georesources.eu/', 'FilmMemory - Joint Master of Arts in European Film Heritage, History and Cultures' with URL 'https://www.filmmemory.eu/', and 'MSc in Smart Cities and Communities' with URL 'https://www.smaccs.eu/'. The fourth result is 'European Master For Industry in Microwave Electronics and Photonics' with URL 'https://www.erasmus-mundus.emimep.eu/'.

Tumia Filter by ili kupata program yako unayoitaka au unaweza kuangalia program zote 189 zilizopo kwa mwaka huu (2025/26) kwa kutumia navigation button ya next iliyopo chini kabisa ya ukurasa huu.


Mfano mimi nimetafuta program ya soil science, hivyo nimeandika "soil science" katika sehemu ya "keywords" na baada ya ku search ikaja hivi:

The screenshot shows the Erasmus Mundus Catalogue search results for 'soil science'. The 'Filter by' section on the left has 'soil science' entered in the Keywords field. The main content area displays 'Erasmus Mundus Catalogue (2)' with an RSS feed icon. Below this, it says 'Showing results 1 to 2'. The first two results are: 'International Master in Soils and Global Change' with URL 'https://imsoglo.eu/' and 'Erasmus Mundus Master in Soil Science' with URL 'http://emissmaster.omu.edu.tr/'.

Katika program zilizokuja, moja haipokei maombi mapya (emiSS) kwa mwaka huu (2025/26) (au pia inawezekana bado dirisha lake halijafunguliwa) na nyengine inapokea (IMSOGLO dirisha lake limefunguliwa kuanzia Octoba 1 2024). Bonyeza katika website ya program husika (kwa hapa nitabonyeza <https://imsoglo.eu/> ili nisome maelekezo yanayohitajika kwa program hii) na imenipeleka katika website husika:



Tafadhali soma maelezo yote katika website husika



Kabla sijabonyeza "Apply now" nimepitia kila 'tab' ikiwemo ya Programme:

imsoglo.eu/programme/

YouTube Maps News watch Gmail MyDownloadTube [...] ADMISSIONS New Tab All Bookmarks

IMSOGLO ABOUT IMSOGLO | PROGRAMME | ADMISSION & APPLICATION | SCHOLARSHIPS & FEES | QUESTIONS | CONTACT | PARTNERS | TESTIMONIALS APPLY NOW


Programme

Programme structure and mobility

IMSOGLO is a **2-year Master of Science** programme containing **120 ECTS credits** and leading to the **joint diploma of International Master in Science in Soils and Global Change**. IMSOGLO is organized by four European universities and involves **mobility** between these partner universities.

The language of instruction is **English**.

IMSOGLO students jointly follow the 1st semester at Ghent University to obtain and supplement their **fundamental soil science knowledge**. The 1st semester is kicked off by the 1-week joint **Primer Event** during which students are introduced to the programme, and get to know each other and staff members of all four partner universities.



Ikiwemo 'Admission & Application':

imsoglo.eu/admission-application/

YouTube Maps News watch Gmail MyDownloadTube [...] ADMISSIONS New Tab All Bookmarks


IMSOGLO ABOUT IMSOGLO | PROGRAMME | ADMISSION & APPLICATION | SCHOLARSHIPS & FEES | QUESTIONS | CONTACT | PARTNERS | TESTIMONIALS APPLY NOW

Admission and application

Admission requirements

Academic requirements

- Academic bachelor degree (minimum 180 ECTS credits or equal) in pure or applied sciences (e.g. chemistry, biology, geology, physical geography, geo-ecology, civil or agricultural engineering, environmental or agricultural sciences, etc.) or an equivalent level from a recognised university or engineering college.
- The obtained bachelor degree must contain at least 40 ECTS credits or equal in natural sciences, covering at least four of the following disciplines: physics, chemistry, mathematics, ecology, biology, geology, physical geography, environmental sciences and agricultural sciences.
- The grades obtained during the bachelor degree must be very good or



Maelezo ya namna ya kuomba utayapata ktk section hii, mfano: Hapa wameelezea kuwa kuna "IMSOGLO application manual" ambayo ni muhimu kuipitia kabla hujaanza maombi yako. Pia wameelezea mambo watakayoangalia ni Academic merit, CV and Motivation. Na matokeo yatatoka kabla ya April 2025.

imsoglo.eu/admission-application/

YouTube Maps News watch Gmail MyDownloadTube [...] ADMISSIONS New Tab All Bookmarks

IMSOGLO ABOUT IMSOGLO | PROGRAMME | ADMISSION & APPLICATION | SCHOLARSHIPS & FEES | QUESTIONS | CONTACT | PARTNERS | TESTIMONIALS

APPLY NOW

How to apply?

Process

- Applications for IMSOGLO student intake September 2025 will open in October 2024.
- All instructions on how to apply and a link to the application portal can be found in the **IMSOGLO Application Manual**.
- Carefully read and follow all instructions in the Manual while completing your application form.

Deadlines

Important

Admission and scholarship selection

The IMSOGLO Student Selection Group, with representatives of all partner universities, grants admission to IMSOGLO based on the academic and language requirements described on this page. Scholarships are awarded by ranking all applications based on previous academic achievements, CV, and motivation. Applicants will be notified about the outcome of the scholarship selection before April 2025.

Appeal

Ikiwemo 'Scholarships & Fees':

imsoglo.eu/scholarships-fees/

YouTube Maps News watch Gmail MyDownloadTube [...] ADMISSIONS New Tab All Bookmarks

IMSOGLO ABOUT IMSOGLO | PROGRAMME | ADMISSION & APPLICATION | SCHOLARSHIPS & FEES | QUESTIONS | CONTACT | PARTNERS | TESTIMONIALS

APPLY NOW

Scholarships and fees

Programme participation cost

The programme participation cost must be paid yearly prior to enrolment and includes tuition fees, insurance and participation in all teaching activities of the programme, including lab courses, excursions, and the master thesis research.

<p>4,500 euro per year</p> <p>for nationals of European Economic Area (EEA) countries (all EU countries + Iceland, Liechtenstein, Norway)</p>	<p>9,000 euro per year</p> <p>for nationals of non-EEA countries (all other nationalities)</p>
--	---



Ikiwemo 'Questions', 'Contact', 'Partners' and 'Testimonials'

imsoglo.eu/partners/

YouTube Maps News watch Gmail MyDownloadTube J... ADMISSIONS New Tab All Bookmarks

IMSOGLO

ABOUT IMSOGLO | PROGRAMME | ADMISSION & APPLICATION | SCHOLARSHIPS & FEES | QUESTIONS | CONTACT | PARTNERS | TESTIMONIALS

Partners

IMSOGLO is jointly organized by a consortium of 4 renowned European universities that was established in 2018:

- Ghent University (Belgium)
- BOKU University (Austria)
- University of Göttingen (Germany)
- Aarhus University (Denmark)

The Consortium Partners are highly complementary in both geographical focus and disciplinary expertise of their research.


Aarhus University and Ghent University work on arctic soils; Ghent University, BOKU University and the University of Göttingen work on tropical soils; and all partner universities work on temperate soils.

Na ndivyo ninavyokushauri, hakikisha kabla hujaanza kuomba basi umepitia maelekezo yote kuhusu program husika. Hii itakusaidia kujua vyuo gani vinashirikiana ktk program husika na modules husika na credits zake, pamoja na kujua kuhusu Interview. Lakini pia itakusaidia kujua nchi gani utaanza masomo yako na nchi gani itafata mpaka unamaliza Masters yako. Kama ni mvivu wa kusoma maelekezo, itakuwia vigumu kupata scholarship hii na nyenginezo. Kumbuka kuwa scholarships ni investment, hivyo zinahitaji muda wako ili uweze kupata faida ya investment hii.

USHAURI: Iwapo una maswali yahasuyo scholarship hii ya Erasmus mundus, tafadhali jiunge na group la WhatsApp la "Prospective EMA Tanzania" ambapo wanufaika wa scholarship hii wapo na watakusaidia kwa haraka zaidi. Wanufaika wana uzoefu zaidi juu ya scholarship hii kuliko muandishi wa muongozo huu. Kiunganishi cha kujiunga na group kipo katika ukurasa wa mwisho wa muongozo huu.

NAMNA YA KUANDIKA EMAIL (Professional email)

Kuna muda itakupasa kuandika email kuuliza mambo ambayo unahitaji ufafanuzi zaidi iwapo umepitia katika website husika na hujapata ufafanuzi unaotosheleza. Namna ya kuandika email ni muhimu kuzingatia: Andika kichwa cha habari (heading) katika "Subject" na maelezo yako katika "Compose", Anza na salamu, jitambulisha kisha elezea hitajio lako, mfano:



Sampuli ya Barua ya Utambulisho kutoka chuoni, (kama bado hujamaliza)

Name: _____
Reg no: _____
Email: _____
Phone: _____

Date: _____

Directorate Of Undergraduate Studies,
University Of Dar Es Salaam,
P.O.BOX 35091,
Dar Es Salaam-Tanzania.

Dear Sir/Madam,

REF: REQUEST FOR LETTER OF INTRODUCTION.

Aforementioned heading is concerned.

I humbly request for a letter stating that I am a University of Dar es Salaam graduate and will receive my University Certificate on a certain date. I urgently need it for scholarship application. My details are:

Name: _____
Reg no: _____
Programme: _____
Department: _____

I will be grateful if this letter is favourably written to further my application, thank you.

Best Regards,

Signature: _____
Name: _____

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmC_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

Sampuli ya Barua ya ngazi ya GPA-Class ranking kutoka chuoni, (kama itahitajika)



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
COLLEGE OF NATURAL AND APPLIED SCIENCES
DEPARTMENT OF MOLECULAR BIOLOGY AND BIOTECHNOLOGY



Date: _____

To whom it may concern:

RE: CLASS RANKING FOR MR/MS. _____

I hereby affirm that, Mr/Ms. _____ is a highly accomplished individual who has consistently demonstrated academic excellence. Mr/Ms. _____ has been recognized for his exceptional performance in both individual assignments and group projects.

With a GPA of __ out of 5, he is ranked in the top __ % of his class. Overall, Mr/Ms. _____ is a true asset to his class and well-deserving of his top ranking.

Thank you for your cooperation.

Dr. _____

Title: _____

Institution: _____

Science Complex Building, University of Dar es Salaam, P.O. Box 35091, Dar es Salaam.

Phone: +255 22 2410500-8, Email: Website: www.udsm.ac.tz

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmc_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

Sampuli ya Barua ya Motisha. Tafadhali usinakili maelezo haya katika barua yako, tumia kukuongoza tu. Iwapo utanakili ndio utakuwa umejinyonga mwenyewe.

Dear Admission Committee,

I am writing to express my strong interest in the Erasmus Mundus Master in Chemical Innovation and Regulation (ChIR) program. With a passion for innovation and sustainability, I believe that this program will provide me with the cutting-edge knowledge and skills necessary to drive positive change in my community.

As the co-founder of Kijani Biotech, a chemical manufacturing startup that focuses on bio-based polymers, With a deep understanding of the potential for biomass valorization to advance economic development, I have developed a business model that benefits local women farmers and provides them with the tools and resources necessary to succeed.

In addition to my entrepreneurial spirit, I am also a leader who values inclusivity and strives to leave no one behind. As the Vice Chairperson of the Microbiology and Biotechnology Students Association, I have organized events that bring together successful figures in the bioeconomy and alumni to share their experiences with current students. Through these efforts, I have motivated others to participate in research contests and shown them what is possible through hard work and dedication.

I believe that my experience in business and leadership, combined with my passion for sustainability and innovation, make me the ideal candidate for the ChIR program. I am eager to gain the knowledge and skills necessary to drive sustainable development in my community through employment creation and equitable sharing of benefits in the value chain.

Thank you for your consideration of my application. I look forward to the opportunity to further discuss my qualifications and enthusiasm for this program with you.

Sincerely,

D. [Signature]

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmC_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

Sampuli ya Uthibitisho wa makazi.

Tafadhali tumia muundo huu kumuonesha Mwenyekiti/Sheha wako aidha uandike wewe au akuandikie yeye lakini lugha iwe ni Kiingereza. Usisahau kuandika anuani ya eneo lako unaloishi.



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION
AND LOCAL GOVERNMENT
ILALA MUNICIPAL COUNCIL
GONGO LA MBOTO WARD



In replying please quote:

Ref. No. **DCC/MT/GMB/VOLA/2023**

Date: ____/____/____

TO WHOM IT MAY CONCERN

RE: CERTIFICATE OF RESIDENCE

Refer to the heading above, I hereby confirm that **Mr./Ms.** _____ born at _____ Hospital in _____ Municipal in _____ city/region on ____/____/____ is a permanent resident of _____ street, living in house number _____ owned by _____.

He is therefore not restricted by this office and may he be served his needs because the _____ Municipal Council authority recognizes him as a permanent resident and responsible citizen.

I express my sincere thanks,

EXECUTIVE OFFICER
GONGO LA MBOTO STREET

Gongo la Mboto Street Local Government Office, P.O. Box **20950**, Dar es Salaam
Telephone: **2128800**, Mobile: **+255 714 134 134**, Fax: 2121486
Email: **info@imc.go.tz**

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmc_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

Sampuli ya barua ya mapendekezo (Recommendation letter).

Hakikisha recommender wako anaandika barua yake kwa kutumia letterhead ya taasisi yake na anaisaini. Tafadhali ongea na uwaombe referees wako mapema na wajulishe kuwa unajiandaa kuomba Ufadhili huu na vyuo vya Ulaya.



LETTER OF REFERENCE

I am pleased to be given an opportunity to recommend Jessica Garcia-Lucas. I have known Jessica as a student of undergraduate studies at the International School of Management, Vilnius, Lithuania. She showed particular interest for multidisciplinary approach to a wide range of issues in the field of International Marketing and related disciplines.

She is highly motivated and her apparent enthusiasm and interest in the subject is supported by his diligent work. By adeptly meeting challenges and showing initiative during our classes, Jessica has shown me repeatedly how dedicated and responsible she is. Her grades have so far been consistently above average and I am certain they will remain so. Jessica is an outstanding individual with a strong character. She is ambitious, determined and creative. She possesses not only a critical mind but she also represents the ideal combination required after in a thorough professional. Her communication and presentation skills are excellent.

Furthermore, I had an opportunity to observe her participation and interaction with other students while he was expressing excellent ability in case study methodology approach for H&M analysis. She was the top 6 in the class of 20 students.

To sum up, I highly recommend Jessica Garcia Lucas for academic or professional development; she will be a great asset of your organization. If you have any further questions regarding Jessica's abilities or this recommendation, please do not hesitate to contact me using the information on this letterhead.

Belgrade, December 15th, 2012

Sincerely,


Vesna Damjanovic, Ph.D.
Associate Professor and Case Study Coach
Visiting Professor, ISM
Faculty of Organizational Sciences, University of Belgrade
e-mail: damvesna@fon.bg.ac.rs
mobile: +381 69 8893 169
<http://rs.linkedin.com/in/vesnadamjanovic>

Jovkova 15/6, 11000 Belgrade, Serbia, Phone: +381 11 3050 800, Fax: +381 11 2461 221
E-mail: dekanat@fon.bg.ac.rs; www.fon.bg.ac.rs

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmc_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

Sampuli ya Wasifu binafsi (CV).

Tafadhali fuata muundo wa Europass. Tumia kiunganishi hiki kujifunza kuhusu Europass CV
<https://europass.europa.eu/en/create-europass-cv>

ions-en.pdf

Open

europass

Instructions for filling in the Europass CV

All CV headings/fields are optional. Remove any fields left empty.

PERSONAL INFORMATION

Replace with First name(s) Surname(s)
If you have more than one first name, start with the one you usually use. Example:
John Smith

Replace with house number, street name, city, postcode, country.
Choose the postal address at which you can be contacted quickly. Example:
32 Reading Rd., Birmingham B26 3QJ, United Kingdom

Replace with telephone number. Replace with mobile number.
Choose the number at which you can be contacted quickly, most likely your mobile phone.
Example:
+44 7871 330 1234

Separate groups of digits in accordance to national convention, to ensure your telephone number is easy to read. Example: +<CountryCode> <AreaCode> <LocalNumber>

State e-mail address:
Choose the e-mail address at which you can be contacted quickly, preferably your personal e-mail address. Avoid fancy or silly addresses. Example:
John.smith@hotmail.com

State personal website(s).
Be sure it is relevant to the position and it does not hinder your application. Example:
www.sample.com

Replace with type of IM service / Replace with messaging account(s).
Be sure it is relevant to the position and it does not hinder your application. Example:
AOL Instant Messenger (AIM) john.smith

Sex Enter sex | Date of birth dd/mm/yyyy | Nationality Enter nationality/-ies

Complete only if required. Check local legal provisions regarding data such as sex, age, nationality, etc. on CV. Example:

Page 2 / 5

Sex Male | Date of birth 01/04/1973 | Nationality Spanish

Source: Danford's shared drive:

https://drive.google.com/drive/folders/1Ek_igdxtDhIxmC_43tlxYfdX1NZLjD (You will meet Danford in the Prospective EMA Tanzania group if you join the group-the group link is within the last page of this document, he's among of Erasmus Mundus Scholars)

KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?

Miongoni mwa yaliyonipelekea kuandaa muongozo huu ni pamoja na kuyaenzi maono ya viongozi waasisi wa Taifa na misingi ya SUZA (SUZA Core values) kama nilivyonukuu hapa chini:

NUKUU KUTOKA KWA VIONGOZI WAASISI WA TAIFA LA TANZANIA.



"Hakuna mtu anayetutaka kuwapenda wengine zaidi ya tunavyojipenda wenyewe, lakini kwa baadhi yetu tuliobahatika kupata elimu nzuri tunawajibika kuboresha ustawi wa jamii tunamoishi, ni sehemu ya kujipenda sisi wenyewe" Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere.



"Jambo moja ni wajibu wetu tukwambieni vijana. Jambo lenyewe ni hili, kwamba msidhani kuwa hii Serekali yenu itaendeshwa na watu wasiokuwa nyinyi. Ni heshima kubwa kila mwananchi leo aliye kijana, aliyesoma mpaka Darasa la nane au kuendelea mbele au asiyesoma nia iwe moja ya kujenga nchi..." Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.



MIONGONI MWA NUKUU 3 KUTOKA KWENYE MISINGI MIKUU YA SUZA (SUZA Core Values)

- + Kupenda na kuchochea mabadiliko katika jamii (Embrace and drive changes)
- + Kuwa na mtazamo chanya kwa jamii (Good intentions)
- + Kuwa mzalendo kwa taifa. (Patriotism)

Lengo kuu la kuandaa muongozo huu pamoja na miongozo mengine ya ufadhili, ni kuongeza uelewa kwa watanzania wenzangu juu ya fursa hizi za ufadhili. Pia kuongeza idadi ya watanzania wanaoomba na wanaochaguliwa katika fadhili hizi.

Pamoja na kuungana na juhudi za watanzania wenzangu waliopata nafasi hizi na wanaowasaidia wengine kupata nafasi hizi.

MIONGOZO MENGINE

Usikose Kufatilia Miongozo Mingine Kama Vile:

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Commonwealth PhD Scholarships
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Commowealth Shared Scholarships
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Chevening
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya China (CSC type A &B)
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya Indonesia (KNB)
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa India (ICCR)
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Erasmus Mundus
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa DAAD scholarships

Na miongozo mengine kadri nitakavyoweza kuiandaa kulingana na uzoefu niliopata wakati naomba fadhili mbalimbali (Fadhili zote tajwa hapo juu niliziomba isipokuwa ICCR). Tafadhali tumia kiunganishi hiki https://drive.google.com/drive/folders/1TfyG9g-YRh1K77ODKIZqd1dNeVXQYBsM?usp=drive_link ili kuweza kuangalia miongozo mengine ya fadhili mbalimbali pindi iwapo tayari.

MPAKA KUFIKIA HAPA SINA ZAIDI YA KUKUTAKIA KILA LA KHERI NA MAFANIKIO MEMA.
NATUMAI MUONGOZO HUU UTAKUFAA NA UTAWAFAA WENGINE.

AHSANTE.

Iwapo utakuwa na maswali na utahitaji msaada tafadhali wasiliana nami kupitia:

mahfoudh.mahfoudh@suza.ac.tz au 0787483930 (Whatsap only)

Au jiunge na kundi sogozi la Whatssap la "Scholarship for Tanzanians" kupitia kiungo hiki:

<https://chat.whatsapp.com/F1L7kVdNALO7NTcUUZbnXP>

Ili kupata msaada wa moja kwa moja kutoka kwa wanufaika wa ufadhili huu wa Erasmus Mundus, jiunge na kundi sogozi la Whatssap la "Prospective EMA-Tanzania" kupitia kiungo hiki: <https://chat.whatsapp.com/B8nlsuxEIM0Inw5Wbi7sQe>

Pia ninakushauri upitie miongozo iliyoandaliwa na watanzania wanufaika wa ufadhili huu (Franklin na wenzako Prince na Edwin) pamoja na muongozo ulioandaliwa na wanaijeria wanufaika wa ufadhili huu kupitia kiungo hiki:

https://drive.google.com/drive/folders/10qFsx0C_fjtC8ArwlsrR9c0JeVnPz_4u?usp=sharing

Ni mimi ninayejali mafanikio yako:

Mahfoudh Mohamed Mahfoudh

School of Agriculture, State University of Zanzibar.

Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa

©2024